# SIKUKUU YA MAVUNO (SHUKRANI NOV. 06/2022)

## NI SIKU YA KILA MTEULE KUONA FAHARI KWA SABABU YA YESU KUWAOKOA. MAANDIKO: ZAB. 124: 1 – 8, 1KOR. 1: 30- 31, YOH. 9: 24 – 33

### 1. UTANGULIZI

Neema hii ya wokovu tuliyo nayo ndugu zangu wamepewa wateule wachache sana hapa Tanzania na ulimwenguni kwa ujumla, ndiyo sababu leo tunakuja mbele zake tukiwa tumejaa mioyo ya shukrani sana mbele zake.

- **Kama kuna jambo ambalo limetufanya tutambe na kutembea kifua mbele, mbele za shetani na majeshi yake bila woga wa aina yoyote, jambo hilo ni wokovu huu ambao tumeokolewa kwa neema tu kati ya mamilioni ya watu. Luk. 10: 21 – 24.**

- **Sote tusikie kweli hii ya ajabu na ya pekee sana anayoisema Yesu Kristo anaisema "Nakushukuru Baba, Bwana wa Mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga, Naam, Baba kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza.**

**"**Maana yake – Yesu alikuwa anashangilia kwamba Baba yake (Mungu Baba) wa Mbinguni hajawapa ufahamu (wokovu) wa kweli za kiroho wale walio na hekima na akili (wasomi) wanasayansi wa ulimwengu huu; bali amefunua wokovu wake kwa watoto wachanga!!! Hili ni jambo kubwa na la ajabu sana ambalo likifunuliwa na Bwana kwa mtu yeyote aliyekuwa na elimu ya dunia hii tu na heshima za dunia tu pia, huyaona mambo haya mengine kuwa kama mavi na kumjivunia Yesu Kristo daima. **Filipi 3: 2 – 11.**

2. Ni nini hasa kilichowapa wateule na watumishi wa Mungu waliotutangulia jeuri na kutamba mbele za shetani wakati wafalme na wenye hekima na akili za dunia hii walipokuwa wamekwama na kukata tamaa kabisa juu ya mambo waliyokuwa wanakabiliana nayo? Wao baada ya kuokolewa na Bwana Yesu (kutengwa) walikuwa wanaona mambo kama Mungu anavyoyaona na kamwe hawakutishwa tena na ibilisi pamoja na vituko vyake.

***Mfano***

a. **2Wafalme 5: 8 – 16** -(Hekima na akili ya kawaida inakataa kwamba kujichovya katika Yordani kunatakasa ukoma!!! Ndiyo Naamani alipuuza, lakini kwa watumishi wa Mungu inakuwa tofauti!!! Hapa ndipo wenye hekima na akili za dunia hii wanapobaki midomo wazi – Haleluya.

b. **2Wafalme 6: 8 – 17, 18 – 23** – Adui na hasira zao, wanapokutana na jeshi la Malaika wanaotulinda wanainua mikono***. Zab. 34: 7.***

- Ngoja niwaeleze leo kwa nini tunamshukkuru Mungu wetu kwa furaha Kuu!! Kwanza pamoja na kwamba tupo katika miili hii, na tunaishi Arusha - Tanzania, kwa hakika kabisa tunaishi katika Ulimwengu (Tanzania) nyingine kabisa ya kiroho isiyoonekana kwa macho haya ya nyama, tunaishi mahala ambapo majeshi ya malaika yametuzingira na yanatuhudumia kwa kiwango cha juu sana. **Mwnz. 32: 1-2, Isay. 63: 7– 9.**

- **"MWAMBIE MWENZAKO" Siyo kwamba tu Mungu yuko upande wetu kama ilivyoandikwa katika Math. 28: 20 na Rumi 8:31; Bali siku zote na saa zote na kila dakika hadi sekunde; jeshi la Malaika linajizatiti kutulinda; liko makini wakati wote kuhakikisha kwamba vita ya aina yoyote inayoinuka kinyume na wana wa Mungu inadhibitiwa.**

**c.** Ndiyo sababu Petro na wenzake waliona fahari kunena habari za Yesu bila woga hata mbele ya Wafalme pamoja na Wakuu wa dini waliowadharau kwamba hawana elimu. **Mdo. 4: 5-22; Mdo. 5: 17-33, 41- 42.**

Nasema wazi kwamba Mungu ameweka neema ambazo hatukustahili kabisa ndani yetu,tunatakiwa kumshukuru kwa dhati kabisa.

(Kama ambavyo Elisha alikuwa analindwa kwa ajabu mno na Malaika wa Bwana na akaendelea kuwa salama; kama ambavyo Malaika walivyomtoa Petro katika hali ya kufa pamoja na mateso mengine mengi **(Mdo. 12: 1 – 11)** ndivyo ambavyo Mungu ameendelea kutenda kwetu sisi watoto wake tuliopo duniani bado. **Yoh. 17:15.**

3. Leo ni siku ya kumshukuru Mungu wetu (Yesu wetu) ambaye ndiye fahari yetu. **Zab. 20:7**

- Unajua, ilikuwa na sheria ya wana wa Israeli kila wanapokwenda kupigana na adui zao; Kuhani alitamka maneno mazito ya ushindi kwa maneno hayo walisimama na kushinda vita vyao vyote. **Kumb. 20: 1- 9** (waliona fahari kwenda vitani na Bwana. **2Nyak.20:20-30; 2Nyak. 32: 20 – 22.**

- Wana wa Israeli waliheshimu sana sikukuu hii ya mavuno (shukrani) na walihama kabisa majumbani mwao na kukaa katika mahema) ili kukumbuka jinsi walivokaa miaka 40 katika mahema jangwani-**Law. 23:34, Lawi 23: 34, 41 – 43. Kumb. 16: 13 – 17.**

  Na tena katika sikukuu hii hakutakiwa mtu yeyote ambaye atatokea mbele za Mungu akiwa mikono mitupu**. Kumb. 16: 16 – 17.**

- **Tumepigana vita vingi tangu Januari hadi sasa, na katika vita vyetu yote tulimweka Yesu mbele na**

**ametushindia, tumefanya shughuli zetu tangu januari hadi sasa, na Bwana ametufanikisha kwa jinsi ya ajabu, leo ni siku ya kila mmoja wetu kumwambia Bwana kwa vitendo kwamba hivi nilivyo ni wewe umehusika Bwana !!!**

- Paulo aliona fahari kutiwa alama mwilini mwake kwa sababu ya Kristo - **Gal. 6:7** (Makovu mengi aliyokuwa nayo Paulo katika mwili wake kutokana na mateso aliyopata wakati anamhubiri Kristo; aliyafurahia na kuwatambulisha watu kwamba kwa sasa anayetawala maisha yake ni Kristo na siyo mtu mwingine tena.

- **Mordekai** hakuinama ili kusujudia kitu kingine chochote isipokuwa Mungu wa Israeli - ***Esta 3: 1 – 5,***

- **Daudi** akaona fahari na kujivunia Jina la Bwana wa Majeshi (Yesu) katika mapambano yake yote na majeshi ya adui – **1Samwl. 17: 45 – 54 (Zab. 20:7)**

- Na sisi leo tumekuja mbele za Bwana ambaye **ametutoa** na **kutupigania** na kutuweka hai tofauti na matarajio ya adui zetu; tupo hivi tulivyo leo kwa sababu ya Jina la Yesu Kristo. ***Mdo. 4: 9-12***

**Note: Kama kuna watu wanaojiuliza Leonard Mwizarubi amefikaje hapo; hili ndilo jibu langu – YESU YESU. Amina**

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***06/11/2022***